



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA  
THE HANSARD**

Tuesday, 1<sup>st</sup> August, 2023  
**Third Assembly – Fiftieth Sitting**

*[The County Assembly met at 10:00a.m. at the County Assembly Buildings]  
[The Speaker (Honourable Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

**PRAYERS**

**The Speaker** (Hon. Khatri): You may be seated.

*[Silence]*

Clerk, please confirm if we have quorum?

*[Silence]*

*[Consultations]*

*[Lack of no quorum]*

Honourable Members, under Standing Order 31(2) “if there is not a quorum present when the Chair is taken, at the time appointed for a meeting of the county Assembly immediately after the saying of the prayer the Speaker shall order the bell to be rung for ten minutes and if no quorum is present at the expiration of the ten minutes the speaker may direct that the bell be rung for a further five minutes and if there is still no quorum present the speaker shall adjourn the county assembly forthwith to the next sitting”sergeant- at -arms please ring the bell for ten minutes.

*[Quorum Bell rung for ten minutes]*

*[Consultations]*

Yes Clerk, please Confirm again if we have quorum?

*[Loud consultation]*

*[Lack of no quorum]*

Serjeant-At-Arms, please ring the bell for further five minutes?

---

*[Quorum Bell rung for five minutes]  
[Lack of no quorum]*

Thank you, Honourable Members...

*[Interruption]  
[Loud consultation]*

Can you count Clerk to confirm if there is quorum?

*[Quorum confirmed]*

Yes, Clerk next Order please?

**COMMUNICATION FROM THE CHAIR**  
VISIT BY STUDENTS FROM SMART START ACADEMY

Honourable Members, the County Assembly is privileged to welcome student and teachers from Smart Start Academy who they include;

1. *Lennox Ouko*
2. *Moses Wambugu*
3. *Dominic Kyalo*
4. *Saad Awadh*
5. *Said Karama*
6. *Akram Karama*
7. *Noel Munyi*
8. *Lugman Mohammed*
9. *Ali Swabri*
10. *Ali Alezadra*
11. *Isaac Munyao*
12. *Tarik Salim*
13. *Sheikha Ahmed*
14. *Ivy Wanjiru*
15. *Bilha Hellen*
16. *Natasha Jumba*
17. *Blessing Kathure*
18. *Mitchel Akinyi*
19. *Aisha Mohammed*
20. *Valleria Busolo*
21. *Baquees Ali*
22. *Sharon Mburu*
23. *Mariam Omar*
24. *Zulfa Ismail*
25. *Ahmed Abdunnassir*
26. *Hashim Iddi*
27. *Hellen Achisa*
28. *David Wambua*

29. *Titus Musyoka*
30. *Chidi Rashid*
31. *Lenny Wanjohi*
32. *Seif Abdul*
33. *Peter Nzioki*
34. *Mirsan Ahmed*
35. *Favour Nkirote*
36. *Zeinab Athman*
37. *Venesa Njeri*
38. *Valary Muthoni*
39. *Abigael Gakenia*
40. *Sheikha Mohammed*
41. *Quinter Ngele*
42. *Faith Kasanga*
43. *Jamal Said Hamisi*
44. *Adrian Kimtai Maritim*
45. *Nurdin Mawiya*
46. *Peter Kasanga*
47. *Emmanuel Baraka*
48. *Patrick Kamau Wanjiku*
49. *Lennox Ibrahim*
50. *Grace Wanjiru*
51. *Abdalla mohammed*
52. *Ann Njeri*
53. *Shekha Yahya*
54. *Yusra Mohammed*
55. *Olivia Kaphaz*
56. *Sarah Buya*
57. *Angel Nyawa*
58. *Issah mohammed*

And teachers are;

1. *Mr. Athman*
2. *Mr. Kevin*
3. *Mr. Thadeus Onsare*
4. *Mr. Robert*
5. *Mr. Aggrey Juma*
6. *Madam Hellen*
7. *Madam Mitchel*
8. *Madam Triza*

*[All names read and bowed before the House]  
[Applause]*

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you very much for coming to the County Assembly...

*[Applause]*

And I hope that with the proceedings you will gain something from these proceedings. Thank you *na Karibuni sana. Ahsanteni.*

*[Applause]*

Clerk next Order please?

### MOTION

ADOPTION OF REPORT ON THE VETTING OF MR. HAMID NANDA THE NOMINEE FOR THE POSITION OF CHIEF OFFICER BLUE ECONOMY, AGRICULTURE AND LIVESTOCK

Yes, Honourable Patrick Mbelle, Chairman Committee on Blue Economy, Agriculture, Fisheries and Livestock, please move the Motion.

**Hon. Mbelle:** Thank you Mr. Speaker Sir. First of all, Mr. Speaker I wish to welcome this team; the children that have visited us today, I wish to motivate them that this is just but a site visit where you have come to learn but know that there is more that you can do out there! Leadership is not just for the young or old it is for all and you can start leadership from wherever you are from school am sure you will lead the world towards the better place in future. Secondly, Mr. Speaker Sir I would wish to move the following Motion;

*THAT, this House adopts the Report on the Vetting of Mr. Hamid Nanda, the Nominee for the position of Chief Officer Blue Economy, Agriculture and Livestock as laid on the Table Tuesday, 25<sup>th</sup> July, 2023.*

I would wish to ask Honourable Pamela Ojala to second this Motion.

**Hon. Arwa:** Thank you Mr. Speaker Sir, I stand to second. Thank you.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Members. Honourable Members, I now propose the question that the Motion by Honourable Patrick Mbelle on Adoption of Report on the Vetting of Mr. Hamid Nanda for the position of Chief Officer Blue Economy, Agriculture and Livestock be considered by this House in the same terms.

*[Question proposed and agreed to]*

Yes, Honourable Patrick Mbelle, please make your contribution to the Motion.

**Hon. Mbelle:** Thank you Mr. Speaker Sir. Mr. Speaker Sir, as read on 25<sup>th</sup> July, 2023 we lay a Paper here for the nomination of one Mr. Hamid Nanda who is supposed to be, if we all agree to allow him to serve in this County as the Chief Officer of this Department of Blue Economy, Agriculture, Fisheries and Livestock. Mr. Speaker Sir, I would wish to ask my fellow Members, I ask my fellow Members to help this department pass Mr. Hamid Nanda to serve in the Department. One thing that I have I personally read and learnt from this gentleman is that he has been in the information technology sector for quite a long time and has in one or two instances been able to rub shoulders with matters pertaining the Blue Economy. At this particular moment Mr. Speaker Sir, the Blue Economy being quite new phenomena in Mombasa County and Coast at large.

Fishing and matters of Blue Economy have been there since time memorial, it is a time that we need somebody who has the right capacity and literacy in matters of information dissemination and gathering so that we will be able to teach and inform our people right in the grass root on what this Blue Economy is about. So, I personally think and acknowledge that this is the right person to guide us through the freshness of the Blue Economy and he will help us here, the team towards the right direction though I wish to invite my fellow Members to support us and pass Mr. Hamid Nanda. Thank you, Mr. Speaker Sir.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you Honourable Patrick Mbelle for your contribution. Yes, Honourable Samuel Mwaura please make your contribution as well you can welcome the student and the teachers.

**Hon. Mwaura:** Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity just to contribute on the Motion, but even before then I am privileged this morning to welcome the students from a school in my Ward Smart Start school from Kongowea. Let me appreciate them for visiting us, let me appreciate the teachers for making it possible for the students to come and learn in this Assembly, it is a privilege to welcome you Sir. Thank you. Mr. Speaker, I have in most cases stood to support Motions in this Assembly but I am afraid I stand to oppose this Motion. Mr. Speaker I am looking at the qualifications of the nominee and indeed he holds a Bachelors Degree but at times we should look at the qualification and what has that person done that qualifies them to hold a certain position. This particular candidate I have looked at it he holds a Bachelor Degree for Commerce and a Diploma in Information Technology Mr. Speaker, I do not know how this is in line with the job that he is going to do concerning the Blue Economy and Agriculture. So, Mr. Speaker yes, he has worked in several institutions that might have informed the decision of the Committee to appoint that nominee and approve him for the position but when we look at those academic qualifications at times, I beg to be guided whether is the right person to hold that docket so I oppose.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Samuel Mwaura for your contribution. Yes, Honourable Solomon Ngugi please make your contribution.

**Hon. Ngugi:** Ahsante Mheshimiwa Spika nikaribishe shule inayotoka eneo Bunge la Nyali, Kata Ndogo ya Kongowea katika Bunge hili letu karibuni niwaambie mko na bahati Kata Ndogo ya Kongowea imebahatika imepata Mheshimiwa wa Kuteuliwa mimi nimechaguliwa kansela maalum lakini eneo la Kongowea ndio sehemu ninayotoka, vile vile Chief Whip wetu pia kizazi chake bali mume wake anatoka Kongowea sasa Kongowea mjue mko na nguvu nyingi ziko hapa Bungeni za kuwasaidia nyinyi msome na bidii nanyi mpate kuiga mifano mema kutoka kwetu manake uongozi unanza kwenu na nina uhakika uko shuleni kuna maprefect wako ma monitor na ukianza Shule mfano mzuri kuwa kiongozi hadi kesho unaweza kuja kuwa kiongozi. Pili, Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga Hoja mkono ilioko mbele yetu hapa. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Nyota please make your contribution?

**Hon. Hamisi Nyota:** Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. First of all, I would like to welcome the pupils from the Smart Start Academy to this House for a learning session, *nasema karibuni sana.*

This is because I know some of them from there, I know there is a future Speaker of this great County of ours and some are Members of this County Assembly. Therefore, I would just give you a small advice; work hard, work smart, be attentive and aim to your goal. Mr. Speaker, I would also love to contribute to this Motion and I stand to support Mr. Hamid Nanda for this position happening to be one of the Committee Members of this Blue Economy. We vetted this gentleman and he expressed vast knowledge on the matters of Blue Economy as a whole and we feel when he is given such an opportunity Mr. Speaker he is going to take this docket to greater heights. Mr. Speaker, no one was born knowing everything; there are those people who learn on the way as they go on with their lives, so I would urge this House to give this gentleman opportunity to work in this docket because there is always a room for someone to learn in life. So, Mr. Speaker we should not judge somebody because he has done ACCA you think that person cannot fit in the other docket. Mr. Speaker in as much as he is learned and i know he is willing to learn more and more so I will go contact my colleague Honourable Mwaura that because this individual he did not go through Agriculture or Blue Economy sector or learning courses he is not fit; he is not qualified to carry this docket for what. Mr. Speaker he is the right individual we vetted him in that Committee room and he expressed willingness and knowledge that once given this opportunity he will take this docket on greater heights. Mr. Speaker, I stand to support and I urge fellow Members to give this gentleman a chance to move Mombasa County forward. Thank you so much Mr. Speaker.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Member. Honourable Deputy Majority from Mtopanga please make your contribution, Minority Leader?

**The Leader of Minority** (Hon. Matsaki): Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza nashukuru Mungu kwa nafasi hii, nashukuru pia kwa Waheshimiwa wenza kufika Bunge hili la leo, karibuni sana watoto wetu, wajukuu wetu wa shule ya Wadi ya Kongowea mjisikie huru na msome na nina matumaini ipo siku baadhi yenu mtakuwa kama sisi hapa karibuni sana na walimu. Mimi nimesimama Bunge hili kwanza kupinga uteuzi wa huyu Bwana...

*[Applause]*

Niko na sababu mbili hasa ambazo mimi ningependa kuziongea na kwa nini napinga; jambo la kwanza Mheshimiwa mwenzu Mwaura ameongea hilo jambo kuhusu elimu ni vyema sana kwanza kulingana na karne yetu unapoamua kupeana kazi ni muhimu hasa elimu iambatane na ile kazi, wewe una mambo ya mahesabu sisi tunaongelelea mambo ya ukulima ni mambo ambayo hayaambatani. La pili ukiangalia utendaji kazi wake haufurahishi mno yeye ni wa kuingia kazini siku mbili tatu, miezi miwili mitatu yuatoka yuaenda kwengine je kweli huyu hata unapompata kazi hii ataweza?! Yuko tayari kweli kufanyia wananchi wa Mombasa Kaunti?! Kwa hivyo mimi nimesimama na nazidi kuisitiza ya kwamba ninapinga uteuzi huu. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Jactone Madialo please make your contribution?

**Hon. Madialo:** I want to take this opportunity to thank you Mr. Speaker Sir. Before I give my contribution, I would also like to declare some interest in a manner; my sister was also interviewed in this department and unfortunately, she was not shortlisted, so I want when making my contribution it goes to record.

Having listened to my good brother Mwaura and also the Minority Leader I am also a bit convinced I think going forward in giving positions such as these we should always give in accordance to one's educational background and also career but also having declare my interest I neither support nor oppose. Thank you.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Fadhili Makarani, Deputy Speaker?

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii kuongea kuhusu mjadala ambao uko mbele yetu. Kwanza kama mimi nachukua fursa kuwakaribisha watoto wetu kutoka Smart Start Academy nawaomba na nafurahi kwa kuwa wako hapa pamoja na sisi ile kuja kusoma yale ambayo sisi kama viongozi tunaowawakilisha tuko hapa tunatekeleza majukumu yetu Mheshimiwa Spika. Vile vile tuna imani ya kwamba ni viongozi wa kesho kama sisi tulivyokuwa watoto Mheshimiwa Spika tulikuwa tukiambiwa watoto ndio viongozi wa kesho na tunashukuru Mwenyezi Mungu kesho yetu Mheshimiwa Spika tumeiona maana tulivyokuwa tunaambiwa hivi sasa ni viongozi na wao pia panapo majaliwa watakuja kuwa viongozi. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kwanza kutofautiana na ndugu zetu kutoka United Democratic Alliance (UDA) Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika ndugu zetu wanajaribu kupotosha Nyumba yetu hii kwa kusema eti kuwa ndugu yetu anataka kusimamia idara ya kilimo Mheshimiwa Spika ati kuwa masomo yake hayalingani na yale ambayo utekelezaji atakayokuja kutekeleza huku Mheshimiwa Spika hayo mimi nitasema ni uongo na wanapotosha kwa sababu Mheshimiwa...

*[Interruption]*

**The Speaker** (Hon. Khatri): Yes, Honourable Mwaura are you on a point of information?

**Hon. Mwaura:** Mheshimiwa Spika ningependa tu kumjulisha Mheshimiwa Fadhili our able Deputy Speaker kwamba hatukuzungumza kama UDA tulizungumza kama Wabunge wa Bunge la Kaunti ya Mombasa kwa hivyo Mheshimiwa Spika naomba tu aweze kutoa hayo matamshi kwamba tumezungumza kama UDA aseme tumechangia kama Waheshimiwa wa hili Bunge. Ahsante.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you Honourable Mwaura. Yes, Honourable Fadhili?

**The Deputy Speaker** (Hon. Mwalimu): Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nakubaliana kuwa ni Wabunge wa Bunge hili letu lakini kutoka mrengo tofauti na mrengo ule ambao natoka mimi...Mheshimiwa Spika mimi natoka mrengo wa Serikali...

*[Applause]*

Ndani ya Kaunti yetu ya Mombasa na ndugu zetu wanatokea upande wa upinzani katika Bunge letu hili japo kule juu wako katika upande wa Serikali sasa kwa hilo Mheshimiwa Spika...

*[Applause]*

Mheshimiwa Spika, waweze kukubali na pia vile vile narudia tu pale mwanzo kuwa wamekosea ama wanatoa kauli potofu katika Bunge hili ya kusema ya kwamba huyu ndugu yetu sijui hajasomea yale ambayo anakuja kuyafanyia kazi. Mheshimiwa Spika, angalia ndugu yetu *employment record* yake ni mtu ambaye amefanya kazi katika mashirika tofauti tofauti, tangu mwaka elfu mbili na tano mpaka leo, ni mtu amefanya kazi mpaka Zanzibar, ikiwa watanzania wanamthamini ndugu yetu huyu sembuse sisi watu wa Kaunti ya Mombasa. Mheshimiwa Spika, ndugu yetu huyu angalia yuko katika *professional associations* ngapi ambazo ndani ya ripoti imeandikwa; mimi nawaomba hawa ndugu zetu kutoka chama pinzani wajiunge, watuunge mkono tuweze kushikana pamoja tumpitishie ndugu yetu huyu ambaye jina lake limeletwa mbele ya Bunge hili ili Kaunti ya Mombasa iweze kusonga mbele, ama nikirudia namuomba Mheshimiwa Mwaura na Mheshimiwa Matsaki wavuke mpaka waje upande wetu tuunge mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**The Speaker** (Hon. Khatri): Thank you. Yes, Honourable Joshua from Jomvu Kuu Ward. Please make your contributions.

**Hon. Mose:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii pia mimi ili niweze kuchangia. Cha kwanza ningeanza kwa kushukuru Kamati ambapo mimi ni mwanachama tulifanya kazi nzuri; ndugu zangu wawili ambao wamesimama kupinga, ningependa kuwakumbusha namna hii, tunatafuta meneja ama a *Chief Officer* huyu amekuwa katika nafasi za kusimamia kazi ifanyike hata kama ni kazi za kuhesabu sio katika idara hii ya Blue Economy na fisheries, *there is no rocket science, fisheries has been there since time memorial*, ukulima umekuwa huko hata mtoto anajua kupanda mahindi na kuvuna na kuvua samaki *so there is no rocket science*. Sisi tulimuangalia huyu *nominee* na kama Kamati ya uchumi samawati tuliweza kuridhika na vile aliongea na tulimkagua *and he is qualified for the job. I support the Motion*.

*[The Speaker (Hon. Khatri) exited the Chair]*

*[The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani) in the Chair]*

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Ong'au. Yes, Honourable Hamida?

**Hon. Noor:** Thank you, Mr. Speaker. Thank you for giving me the opportunity, I would like to welcome the students from Smart Start Academy from Kongowea and I would like to inform them that I have been nominated twice from Mkomani and you are leaders, you should work hard so that you will become the next leaders of Mombasa County Assembly. Mr. Speaker, I do stand here to support the Motion of the Blue Economy for Mr. Hamid as my colleague have expressed that he has vast experience in his academic jobs that he has done from several places, as you yourself has expressed that he has worked all the way from Zanzibar. So I think he has the opportunity to give us the experience so that we can go forward with the Blue Economy because it's a new thing for us right now and we need to do it because all over the world people are looking into the Blue Economy so that if we get someone like him that we have nominated him in to this docket I think he will give us his verse experience that he has gotten. With those few remarks I do stand to support the Motion. Thank you so much.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Hamida. Yes, Honourable Solomon Ngugi. Honourable Ngugi, you have already talked.

---

**Hon. Ngugi:** I stand on a point of order.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Ngugi let Honourable Fatma Mote.

**Hon. Fatma Swaleh:** *Bismillahi Rahmani Rahim.* Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipa fursa hii; kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi pasi na kizuizi, vile vile ningependa kuwashukuru watu wangu wa Kazdandani kwa kuweza kunifikisha hapa. Mheshimiwa Spika, mimi ni katika wale Waheshimiwa ambao naweza kujivunia ambae niliweza kupigiwa kura bila kuibiwa...

*[Applause]*

Mheshimiwa Spika nimesimama hapa bila kigegezi kumuunga mkono, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbelle na Kamati yake. Vile vile nimesimama kuunga mkono kwamba Hamid ni kijana wa hapa hapa Mombasa na vile vile nimeenda nikiangalia stakabadhi zake anakisoma na elimu ya tajriba ya hali ya juu kwa hivyo Mheshimiwa Spika sina budi kuunga mkono...

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): There is a point, an Honourable Member is up. Yes, Honourable from Chaani.

**Hon. Makanga:** Mheshimiwa Spika ningepomba...

*[Interruption]*

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Have a seat Honourable Kushe.

**Hon. Makanga:** Mheshimiwa Spika ningepomba kwa heshima na taadhima Mheshimiwa wa Kazdandani alieleza Bunge hili anachomaanisha kusema kwamba kuna Waheshimiwa walioibiwa kura amesimama akasema yeye hakuibiwa kura sasa yeye atuambie katika Bunge hili ni nani aliyebiwa kura ili tuwasaidie kupata haki yao.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Yes, thank you. Honourable Kushe can you substantiate.

**Hon. Fatma Swaleh:** Mheshimiwa Spika nimejizungumzia mimi mwenyewe manake najua ameingia hapa kihalali na naomba unilinde maana sijataja Mheshimiwa yeyote kwamba ameibiwa kura hapa na mfano mmoja tu, Mheshimiwa Raila aliweza kuibiwa kura...

*[Applause]*

Kwa hivyo mimi nimeingia hapa sikuibiwa kura Mheshimiwa Spika na najivunia na yani nawapa shukurani watu wangu wa Kazdandani, na sidhani kama kuna kosa. Bwana Spika?

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Yes Proceed. Yes, Honourable Mwaura?

**Hon. Mwaura:** Mheshimiwa Spika, nafikiri kama jinsi Mheshimiwa mwenzake amesema hata hayo maswala ya kwamba Mheshimiwa Raila aliweza kuibiwa kura anafaa kuyadhibitisha na kusema jinsi hiyo kura ilivyoibiwa na kusema ni nani aliyemuibia ili tuweze nasisi kuelewa, asiseme maswala ya watu ambao hawawezi kuja kwa hili Jumba kujitetea na kusema ni kweli ama si kweli lakini yeye pia anaweza kuji substantiate Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Hamida before I return it to Honourable Fatuma Mote.

**Hon. Noor:** Mr. Speaker Sir, I think we are getting out order because what we have come here to debate on is the nominees for the Chief Officer but not to get in to other debates because we are here to pass the nominees for the Chief officer, that is what I wanted to clarify to the House. Thank you.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you for that information that the Hon. Member she has stated a statement and now the other Members want her to substantiate on what she said, it is not a new Motion so Fatma please substantiate on what Honourable Mwaura has raised.

**Hon. Fatma Swaleh:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza Mheshimiwa Spika nashangaa kwa nini Waheshimiwa wenza wanaduku duku na wasiwasi mimi narejelea tena kusema mimi nimeingia hapa kihalali na kama kweli wao wanauchungu, server ingefunguliwa...

*[Applause]*

Maadamu *server* ilishindwa kufunguliwa mimi nina hakika Bwana Mheshimiwa Raila Amollo Odinga aliweza kuibiwa kura Mheshimiwa Spika. Tuendeleo kwa mada Mheshimiwa Spika ukiangalia stakabadhi za Hamid ni kijana ambaye ana elimu na hekma ya ana tajriba ya hali ya juu Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo sina budi kuunga mkono na kuipitisha. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Florence, before Honourable Florence, what is it Honourable Mwaura.

**Hon. Mwaura:** Mheshimiwa Spika ni vizuri Mheshimiwa Kushe amesema, Fatma Mote aweze pia kuthibitisha kwa sababu amesema server hazikufunguliwa na yeye alipita halali, mimi sijui *server* iliyomchagua iliweza kufunguliwa ama baado mpaka leo haijafunguliwa.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Fatma have a seat. Let us proceed with our Motion. Yes Florence?

**Hon. Kachumbo:** Thank you Mr. Speaker for this opportunity to share my views. First of all, I would like to welcome the students from Smart Start Academy group, I remember like I said last session when I was still in primary we were also taken to the National Assembly and when I was there, I did not know that I would become a leader one day. So, do not be afraid to aim high be open because the sky is the limit, on to today's report Mr. Speaker I would like to differ with my colleague from the other party I do not agree with this report.

I beg to differ when you look at his employment records, you see he is a learned man but he has experience more on the financial department, when you look at this department it is for the Blue Economy Agriculture and Livestock and fisheries you see he is not quite conversant with the roles accorded to this department so I wish to differ and I disagree with this report. Thank you.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Florence, the Majority Leader is up so proceeding Majority Leader.

**The Majority Leader** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika niungame na Waheshimiwa wenza kuwakaribisha wanafunzi wetu na vile vile kuwausia tu ya kwamba kila mwanaadamu lazima awe na malengo katika dunia hii na ufanisi katika malengo. Mheshimiwa Spika, lazima uwe na ghera yako na ni bayana ya kwamba kila mwenye kujitahidi hupata, hivyo basi niwausie tu wanafunzi hawa kwamba waiweke katika akili yao na mioyo yao jitihada kwa sababu mwisho wa siku, jitihada pekee ndio huleta ufanisi. Mheshimiwa Spika, wengine huzungumzia kuhusu bahati lakini hii bahati ni ya Maulana kwa amtaakae lakini kwetu kama wanaadamu tumeusiwa kujituma, tumeusiwa kujitahidi ili tuwe na yakini kiufanisi katika yale tunayo pigania. Mheshimiwa Spika, tukirudi katika hoja binafsi ni Mwanakamati katika Kamati hii ya Uchumi Samawati, kilimo na ufugaji na jukumu letu ilikuwa ni kumpiga msasa ama kumfanyia uchunguzi mteule huyu na kuleta ripoti katika Bunge hili ili waweze kumpitisha ama kumkatalia.

Lakini Mheshimiwa Spika, tukirudi katika muongozo wa jukumu hili kwa mujibu wa sheria tukienda katika sheria za Ugatuzi sheria za Ugatuzi sheria ya 45 inatuambia sehemu ya kwanza kwamba ni Mstahiki Gavana miongoni mwa wateule wengi kupitia kwa mfumo wa mchujo, *competitive* wa mashindano ambao husimamiwa na Bodi ya Huduma za Umma katika Gatuzi letu. Wao ndio hufanya tathmini wakapendekeza miongoni mwa majina yaliyoletwa ni nani anaestahiki na Gavana kuchagua mmoja na kuleta kwetu kwa ajili ya kupitisha ama kuangusha. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika vigezo vinavyo stahiki kuangaliwa vinaanza kule kwa County Public Service Board ama kwa Tume ya Huduma ya Umma za Gatuzi letu na si kwetu sisi. Pili, Mheshimiwa Spika tukija katika jukumu letu sisi la kupitisha ama kuangusha kwa kisingizio kipi, moja tumezungumzia kuhusu maswala ya tajriba ya muhusika ama mteule lakini pia niwaulize Waheshimiwa wenza...

[*Interruption*]

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Order Honourable Members!

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Ni waulize Waheshimiwa wenza ambao wanapinga; ya kwamba hivi katika fahamu zao timamu, wana ufahamu majukumu ya afisaa mkuu? Mheshimiwa Spika, afisaa mkuu anatekeleza majukumu shikilizi, majukumu ya kuazimwa, mamlaka ni ya baraza katika Gatuzi ambalo baraza hili ni Gavana na mawaziri wake chini ya waziri ndio kuna watu wanaitwa maafisaa wakuu wanatekeleza majukumu ama mamlaka ya kuazima. Mamlaka haya yako kwa waziri, kwa hivyo Mheshimiwa Spika swala la kujiuliza je, tunae waziri mwenye vigezo katika idara inayostahiki? Kama ndio, afisaa Mkuu ana tekeleza amri kutoka kwa waziri wake mheshimiwa Spika, kwa hivyo kwanza Waheshimiwa wenyekupinga walifahamu hili. Pili, Mheshimiwa Spika Afisaa mkuu, waingereza wanaita *Accounting Officer* yeye ndie anaeshikililia *vote book* ambayo katika maswala ya *vote book* imebeba maswala ya mahesabu ambayo moja kwa moja katika kuwezesha swala hili.

Ni lazima uwe na vigezo vinavyo ambatana na elimu ya uhasibu Mheshimiwa Spika, kwa hivyo kama ndugu yetu kasoma maswala ya hesabu, ni mwanahesabiya, ni mwana mahesabati, hakuna dharura wala uharamu wake yeye kuwa Afisaa mkuu. Kwanza ni faida zaidi katika nafasi ile ikiwa anautaalumu na maswala ya mahesabu na fedha Mheshimiwa Spika, kwa hivyo hii nampa nafasi bora zaidi kuliko yule aliyesomea maswala ya uchumi samawati lakini si mtaalam ya maswala ya hesabati, hivyo basi hii nampa alama zaidi katika kushika nafasi ile....

[Applause]

Mheshimiwa Spika pia sheria ya ugatuzi inampatia Mstahiki Gavana katika sehemu ya nne mamlaka, sehemu ndogo ya tano inampatia mamlaka ya kugeuza ama upangilia upya nafasi katika hiyo. Kwa hivyo leo Mheshimiwa Spika ataingia afisaa mkuu akiwa amesomea taaluma ya uchumi sawati lakini Gavana sheria inampatia mamlaka katika sehemu ya 45, sehemu ndogo ya tano kumtoa katika nafasi hii na kumuweka katika idara ya elimu, kumtoa katika idara ya elimu kumpeleka katika maswala ya vijana na michezo. Hii kuwepo kwake haiambatani ama hakuna kisingizio cha yeye kutofaulu kuwepo pale kwa sababu ya kwamba hajasoma maswala ya uchumi samawati. Hivyo basi Mheshimiwa Spika, niwahimise Waheshimiwa wenzi kama walivyo jitokeza na maoni mbadala wanatoka upande wa kile chama chengine. Sisi tukiwa hapa kama serikali na ni wajibu wangu pia nikiwa mkongwe kiasi cha haja Mheshimiwa Spika kuwakumbusha ndugu zangu wa UDA ya kwamba wawe na mazoweza angalau mara kwa mara kabla ya kuja na hoja waangalie hoja zao je zimekwenda shule ama wanachangia kwa minaajili ya kuchangia na wao kuhesabika katika kumbu kumbu za Bunge hili kuwa walichangia. Ahsante Mheshimiwa Spika, naunga mkono na nawasihi Waheshimiwa wenza tuweze kuunga mkono ndugu yetu na kusonga mbele. Ahsante Mheshimiwa Spika...

[Applause]

**The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani):** Yes, Honourable Makanga?

**Hon. Makanga:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika na nianze kuwakaribisha wanafunzi kutoka eneo Wadi ya Kongowea na nasimama mimi binafsi kuunga mkono hoja hii kwa sababu zifuatazo; kuanzia mahali alizaliwa mimi nimeangalia na kati ya vitu ambavyo mimi vinanisukuma kufanya maamuzi ni kwanza huyu mtu je anaelewa maswala ya Mombasa? Na kama anaelewa maswala ya Mombasa ameyaelewa kwa kuhadithiwa ama kwa kuwa ni mkaazi na mzaliwa wa hapa? Kwa hivyo Mheshimiwa Spika hilo ningekuwa Mheshimiwa yule mwenye kupeana asilimia, tayari angekuwa na asilimia hamsini amezaliwa katika jimbo la Mombasa, mnamo tarehe 31/5/1983. Mheshimiwa Spika, nimeweza kuangalia sheria zote zinazohusiana na uteuzi wa *Chief Officer* na nimegundua kwamba hakuna mahalo popote panaposema ya kwamba lazima ateuliwe kwa idara ambayo ama kwa maswala ambayo amesomea. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika wale wanao simama kupinga labda tu kwa kufurahisha nia zao na nafsi zao lakini hawana sababu ya kisheria ya kupinga! Mheshimiwa Spika, huyu ni mzaliwa, huyu ni mpiga kura na hivyo ana haki kabisa kama mkaazi wa Mombasa kupata nafasi hii ili aweze kuihudumia jamii yake ambayo yeye pia ni mkaazi. Mheshimiwa Spika, ukiangalia pia katika maswala ya masomo, kusoma amesoma na unajua mgala muue na haki yake umpe na pia hapa uswahilini wakasema mcheza kwao hutuzwa. Huu ni wakati wa kuwatuzwa wakaaji wa Mombasa, wazaliwa wa Mombasa wahudumie wananchi wao kwa sababu hiyo ndio iliokuwa lengo na sababu kubwa ya Gatuzi kuundwa kulingana na katiba yetu ya 2010.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, bila kupoteza muda na bila kukausha kinywa changu, mimi nasimama kuunga mkono na niombe hawa wenzangu pia wanaopinga kama nilivyosema ni haki yao ya kikatiba lakini pia tuangalie tunapopinga kuna sababu ya kimsingi ama sababu ya kisheria ama kuna lolote ambalo labda limepitishwa linalozuia uteuzi wa huyu ndugu yetu Hamid. Kwa hivyo mimi naunga mkono kwa niaba ya wanachaani, ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Kai?

**Hon. Kai:** Ahsante Bwana Spika kwa kuweza kuniruhusu pia mimi nikaweze kuungana na wengine kutoa maoni yangu kutokana na teuzi hii ya kaka yetu ambaye ni Hamid Shehan. Kwanza nataka nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati hii ambaye ni Mheshimiwa wa pale Bamburi jirani yangu Mheshimiwa Patrick Mbelle. Kwa sababu uliweza kutupatia fursa ya kuweza kuhoji yale ambayo tuliweza kuhoji teuzi hii nataka niseme ya kwamba mimi kama Mheshimiwa Syvester Tsuma Kai kwa niaba ya watu wa Junda nataka nichukue fursa hii kusema ya kwamba niliridhika kwa yale maswali yote ambayo niliweza kuuliza kwa yule aliyeteuliwa na nikaweza kuona ya kwamba ana ufahamu wa kutosha katika sehemu hii ambayo ameweza kuteuliwa...

*[Applause]*

Na hivyo basi niuungane na Bunge hili, niungane na wengi kusema ya kwamba tuna imani kubwa sana ya kwamba kwa kumteua ndugu yetu huyu basi kwa mara ya kwanza Uchumi Samawati utaenda kuwa katika zile nyanja ambazo zitaweza kufanyiwa kazi na ziweze kuleta ajira na ziweze kuonekana ya kwamba Uchumi Samawati kitovu chake kiko ndani ya Mombasa. Shukrani sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Sylvester Kai and Honourable Members, that is democracy, an Honourable Member from the United Democratic Alliance, UDA party joining hands with the Members from the ruling party....

*[Applause]*

And supporting the Motion on the floor. Honourable Members, I now take this opportunity to call upon the mover of the Motion to respond before we proceed to voting. Yes, Honourable Patrick Mbelle?

**Hon. Mbelle:** Thank you Mr. Speaker Sir for allowing us to debate on our very own Mr. Hamid Nanda who we as the Committee that I chair thought it was wise to approve his appointment and at this moment I wish also to respect the wishes and words of those that went against the Motion. But again, I think what I have heard from what other Members have said is that probably they might have been other matters and issues political motives as to why they decided to go that way but again I still respect what they said. Mr. Speaker Sir, one thing that I want to remind Honourable Mwaura and others that went against the Motion is that Mr. Hamid Nanda is a progressive gentleman. If you look at his Curriculum Vitae Mr. Speaker Sir, if you would allow me to look at his employment record all the way from 2004 where he started working with his diploma at Overdrive Consultancy as a Computer technician in less than a year he went ahead to become an Assistant Accountant at the Indian Apartment Hotel.

According to what we have read here, is that he had qualified and graduated with his degree in Commerce. Mr. Speaker Sir, a person who is qualified and knows what he does never sticks in one company normally this person in a layman's language is called a hot cake! Every company looks for this person to work with and that is why if you look at his employment record, all the way from Indian Beach Hotel he was poached by our neighbouring country Zanzibar to work for a company called Drop of Zanzibar and still came back to our country; but if you check in 2018 he then went ahead to become a Finance Manager for an East African Company called East Africa Infrastructure Limited. So, this tells you that this gentleman Mr. Speaker is a man of progress, is a man that knows what he does and he is a man will steer the ship of the Blue Economy within Mombasa and probably the Constitution at large in the right direction.

Mr. Speaker Sir, I would also wish to enlighten other Members that until now there is no university offering a Bachelors in Blue Economy; so if you expect to have a nominee that will come to this House with the Bachelors in Blue Economy then Mr. Speaker we would not have any. But again having been a person that has acquired a Bachelors in Commerce and as you all know that Commerce is one sector that brings every sector within this globe to do business then Mr. Speaker Sir am sure with his knowledge and competence in Commerce he is going to help us unlock matters of business within the Blue Economy sector which until now is a sleeping giant within the County Government of Mombasa and our Country in general. Mr. Speaker Sir, with that said I would wish to urge Members both those that oppose and those that went with the grain to support Mr. Hamid Nanda to help us approve him for this position knowing very well that this gentleman will serve both those who are in Azimio and those that are in Kenya Kwanza to better the lives of their parents, to better the lives of their sisters and brothers back at home. This is because the Blue Economy Sector Mr. Speaker Sir, is one Sector that in future it is going to unlock so many opportunities for everyone in this Country. So, Mr. Speaker Sir, with that I would wish to ask all Members respectfully those that oppose and those that I thank for having supported Mr. Hamid Nanda to join me in approving Mr. Hamid Nanda. Thank you, Mr. Speaker Sir.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Patrick Mbelle. Honourable Members, it is voting time now and I now stand to put the question that the Motion by Honourable Patrick Mbelle on Adoption of Report on the Vetting of Mr. Hamid Nanda the Nominee for the Position of Chief Officer Blue Economy, Agriculture and Livestock be approved by this Honourable House in the same term as moved.

*[Question put and agreed to]*  
*[Applause]*

Yes Clerk?

### **MOTION**

ADOPTION OF REPORT ON THE VETTING OF DR. ROSELYNE RANDU THE NOMINEE FOR THE POSITION OF CHIEF OFFICER EDUCATION

Yes, Honourable Allen Katana?

**Hon. Katana:** Mr. Speaker, I beg to move the following Motion:

---

*THAT, this House Adopts the Report on the Vetting of Dr. Roselyne Randu, the Nominee for the position of Chief Officer Education as laid on the Table on Tuesday, 25<sup>th</sup> July, 2023.*

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Who is your seconder?

**Hon. Katana:** I would wish to ask the Honourable my sister-in-law Honourable Pamela to second. Thank you.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Pamela?

**Hon. Arwa:** Thank you Mr. Speaker Sir, I stand to second.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Members, I now propose the question that the Motion by Honourable Allen Katana on Adoption of Report on the Vetting of Dr. Roselyne Randu the Nominee for the Position of Chief Officer Education be considered by this Honourable House in the same terms as moved.

*[Question proposed and agreed to]*

Yes, Honourable Katana proceed.

**Hon. Katana:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi sitakuwa na maswali mengi mpaka wale wapinzani ambao nahisi wametumwa kwa hili watakuwa hawana sababu ya kupinga kwa sababu Daktari huyu anafaa kwa kazi hii. Kwa hivyo mimi ninachowaomba tu ni Waheshimiwa wenza tuunge mkono hoja hii ili mwisho wa kwisha tuweze kupata afisa ambaye atafufanyia kazi. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Milka Moraa Ngare?

**Hon. Ngare:** Thank you Mr. Speaker for the opportunity, may I first take this chance to welcome students and teachers from Smart Start Academy. I love the name, Smart Start...

*[Applause]*

They are starting smart congratulations for starting smart and welcome to our Assembly and I wish you all the best in your studies and I congratulate the teachers for moulding you well. Mr. Speaker, may I take this opportunity to also say that Mr. Katana, Honourable Katana and the team have done a good job on the report on Dr. Roselyn Sidi Randu who is the nominee as a Chief Officer for the Department of Education and Digital Transformation. We need somebody who has credentials like those of Dr. Sidi to run the docket of Education which is very important for our children within the County of Mombasa, because we need somebody who will take the Education standards to a high level and having looked at the credentials of Dr. Sidi, I think she has...

*[Interruption]*

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): What is it Honourable Kai?

**Hon. Kai:** A point of Order!

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): What is the point of Order?

**Hon. Kai:** *[off microphone]*.

*[Interruption]*

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Use your microphone.

**Hon. Kai:** Nilikuwa najaribu kupitia *Members* ambao waliweza kumfanyia msasa na niko na hofu naona ni kama kuna mgeni ambaye si wa Bunge hili aliweza kujumuishwa katika orodha ya *Members*. Kwa hivyo ningetaka labda nifahamishwe ya kwamba je ni mmoja wetu ama huyu ni mgeni na kama ni mgeni aliingiaje? Naomba kutambua kama katika Nyumba hii tuko na mwenzetu ambae anaitwa Mheshimiwa Patrick Mbelle Mumba.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. I think the Chair will respond. Honourable Milka, proceed the Chair when you up on responding you will respond on that.

**Hon. Ngare:** Thank you Mr. Speaker. So, as I conclude, I think the nominee deserves the position; she has a Doctorate of Philosophy of Educational Management from the Moi University amongst many other qualifications that puts her on a higher level than the other nominees maybe who had applied. So, I stand to support and I ask our colleagues to also support the nominee so that we can have things running in the Education Sector. Thank you, Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Manuari?

**Hon. Juma Manuari:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa juma hili la leo, pili niwakaribishe vijana wetu viongozi wa kesho na nawaombea sana Mwenyezi Mungu awape mwelekeo na mwongozo katika maisha yenu ili musiingie katika zile kashifa na madhila ya dunia ambayo saa hizi yanaendelea. Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kumuunga ndugu yangu mkuu wa Elimu wa walimu Ndugu yangu Daktari Allen Katana kwa yeye na Kamati kwa kumteua ndugu yetu Daktari Roselyn Randu na kwa kuwa ni mmoja katika wale watu wasomi kwa sababu mtu ni Daktari. Mimi nampitisha moja kwa moja kuwa yeye anastahili kusimamia katika mwelekeo wa Elimu ndani ya Mombasa yetu. Mheshimiwa Spika, Daktari Randu kama tulivyoisoma katika jedwali hili tulilopewa juma la leo, tumemuona ni mmoja katika wale wana Pwani ambao wako mbele, mstari wa mbele ki elimu. Kwa hivyo ni jukumu letu kama Bunge hili kumpitisha mtu wetu ili kazi zetu ziwe rahisi kwa hayo mengi machache Mheshimiwa Spika namuunga mkono ndugu yangu.

*[Applause]*

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Mwalimu): Thank you. Yes, Honourable Jacktone Madialo?

**Hon. Madialo:** Ahsante sana Bwana Spika kwa kunipatia fursa hii. Ningependa kuunga mkono Hoja hii na pia kumpendekeza huyu ambapo ameletwa mbele yetu ili apate kupitishwa. Langu ningependa kusema hivi, tujaribu kujitoa katika semi ambazo tusipochunga tunapozidi kuendelea zitatugawanya katika mirengo mingi ya kikabila na ya kidini. Kwa hivyo tunapopitisha watu tuwache maneno kama mtu wetu ni mtu wa kila mtu tupitisha watu kulingana tajiriba zao. Ahsanteni.

**The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani):** Thank you. Yes, Honourable Kimari?

**Hon. Kimari:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nianze kwa kuwakaribisha wanafunzi wa Kata ya Kongowea, mimi naitwa Mheshimiwa Eliud Kimari kutoka kata jirani ya Mkomani. Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kuunga mkono Bi. Roselyn Randu kama mteule katika nafasi ya Afisa Mkuu katika Idara ya Elimu. Ukiangalia katika zile *qualifications* zilikuwa zinahitajika utapata kuwa yeye mwenyewe amesoma ana PHD na ukiangalia wale waliokuwa wakimpiga msasa Mheshimiwa Spika nikianza na Mwenyekiti wetu wa Elimu hajasoma kuliko yule...

*[Applause]*

*Candidate mwenyewe ambaye twampitisha hapa Mheshimiwa Spika na...*

*[Interruption]*

**The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani):** There is a point of Order.

**Hon. Hamisi Nyota:** Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker, I am standing on Standing Order No.87, he is misleading this House! Mr. Speaker, my colleague Honourable Eliud Kimari is alleging that Honourable Allen Katana is not as learned as this Chief Officer, but does he know up to what stage Honourable Allen Katana has studied? So, Mr. Speaker I think it is prudent not to mislead this House. Thank you.

**The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani):** Continue Honourable Eliud Kimari?

**Hon. Kimari:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Tukiendelea Mheshimiwa Spika ukiangalia upande wa elimu huyu mteule ni kweli amesoma na ana ambatana ile elimu yake ina ambatana na ile wizara ambayo atakuwa akifanya chini yake. Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika ile Miswada imekuja mbele hapa, mbele yetu ambayo imepita kidogo, kuna zile tetesi lazima ile *degree* uliosomewa lazima iendane na ile wizara. Kwa hivyo hapa hakuna upingamizi wowote upande huo Mheshimiwa Spika ukiangalia upande wa *clearance requirements*, ameweza kupitishwa na KRA, hana deni na CRB hajahusika mahali popote na DCI, EACC hata HELB yenyewe hana deni. Lakini Mheshimiwa Spika kuna mahali nilikuwa tu na duku duku kidogo, pale pa *networth*. Nafikiri katika lugha ya kimombo tuko na wanafunzi hapa, *the ultimate goal* ya kila mmoja wetu hapa ni tuweze kusoma kama wale wanafunzi waweze kusoma na *the ultimate goal*, ukipata elimu ni mafanikio kwa maisha na mafanikio yanakuja upande wa pesa. Mheshimiwa Spika, tukiona mtu ana PHD na ana *networth* ya Ksh 8Million, *at least* inatutia wasi wasi kidogo *especially* kwa hawa wanafunzi walio hapa. Lakini ningependa kuisitiza *even* Jumba zima na waliopo hapa kuwa si kila mtu ambaye anaweza kuwa na PHD na awe na hii pesa inaweza kuwa na uwezekano yeye anapeana kwa jamii ama anachangia kule kwengine.

---

Kwa hivyo nimesimama kuunga mkono Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Kimari, even though you did not substantiate as per the Standing Order No.27 as it was raised by Honourable Hamisi Nyota, so next time adhere to the Standing Order. Yes, Honourable Mwaura?

**Hon. Mwaura:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Naam, Mheshimiwa Spika nasimama kuiunga Hoja hii mkono...

*[Applause]*

Ili ithibitishie ya kwamba hata niliyopinga sikupinga kwa sababu ya chama na misingi mingine, nilipinga kwa sababu ya yale nilioyaona katika uteuzi ule Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Spika Mheshimiwa Madialo amezungumzia swala ambalo ni nyeti na ni la muhimu sana katika Bunge hili; kwa sababu mara kwa mara nimesikia Waheshimiwa hapa katika hili Jumba wakisema huyu anastahili kwa sababu he/she is born and bred in Mombasa. Niwaambie ya kwamba katiba ya nchi hii yetu ya Kenya inaruhusu Mkenya yeyote kuchukua wadhfa na kuchukua nafasi na kuwajiriwa katika Kaunti yoyote katika mji huu na zaidi inasisitiza kwamba, kiwango cha asilimia thelatini ni lazima kiwe kimetoka katika maeneo nje ya ile Kaunti ambayo inahudumiwa. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika maswala ama matamshi mengine ni kweli hayastahili kwa sababu nikiangalia kama huyu ninaye muunga mkono, sasa hivi nikiangalia kuzaliwa kwake, amezaliwa katika Kaunti ya Kilifi Mheshimiwa Spika na ninasema anahaki kabisa ya kupata hii kazi ama huu uteuzikama vile yule aliyezaliwa ndani ya Mombasa ana haki Mheshimiwa Spika.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nataka niseme katika masomo ya huyu daktari, nikiangalia yanaambatana kabisa na ile kazi anayoenda kuichukua; hata zile kazi ambazo amezifanya ni kazi ambazo zinaambatana na ule uteuzi ambao ameteuliwa, amekuwa Mwalimu, amesimamia katika idara ya uwalimu na hii inatupatia ujasiri ya kwamba huyu aliyeteuliwa tunamwita Randu amehitimu ama ana *qualify* kuchukua hii nafasi. Mheshimiwa Spika, huyu amezungumza kwamba hajaingia katika vitengo vya kiusalama na kiuchunguzi ya kwamba, akashutumiwa na kashfa yoyote na Mheshimiwa mwenzangu amezungumzia *net worth*. Nataka niseme nikiangalia huu utajiri wa huyu, huyu ndiye ambaye anaweza kuniambia hata kama anasema hajashutumiwa mahali, anaweza kuniambia kweli nimsafi. Kwa sababu nikiangalia umri wake na ule utajiri ako nao kusema la kweli ninaona hajagusa shillingi kutoka kando ya mshahara wake Mheshimiwa Spika! Wengi wa wale tuliowapitisha walikuwa na miaka michache na mtu ni tajiri zaidi hata ukipiga mahesabu ya ule mshahara, unajiuliza ni wapi alipiga mapande lakini hio ni stori ya siku nyengine tutaizungumza. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nasimama kuunga hoja hii mkono. Ahsante sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Senior Chief Maryam Baimu?

**Hon. Baimu:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza ningependa kuwakaribisha watoto wetu wa Shule ya Smart Start Academy na nasikia inatoka Nyali, kwa hivyo karibuni sana Bunge letu, mujisikie muko huru. Kitu cha kwanza ningependa kuzungumzia Mheshimiwa Spika ni kwamba, ningependa kuunga mkono Mswada huu kwa sababu hata mimi ni Mwanakamati wa hii Elimu. Kwa nini nasema nataka kuunga mkono ama nimeunga mkono?

Kitu ya kwanza tukiangalia huyu *Nominee* Roselyn Randu ni mama, kwanza umri wake amezaliwa mwaka 1966 kwa hivyo kiumri amekomaa vya kutosha na nina imani ako na hekima ya kutosha. Nikienda pia upande wake wa elimu tunaona hapa kuna maneno makubwa makubwa *Doctorate, Masters* na *Degree* zote hizo; kumaanisha hata Birmingham alifika mwenzetu. Kumaanisha huyu katika hii nyanja ambayo anataka kufanya amehitimu vya kutosha, ataweza kufanya kazi nzuri zaidi. Pia upande ule ule wa elimu ningependa kusema hivi; najivunia sana kwa huyu mama Roselyn kwa sababu katika elimu yake ya shule ya upili amesoma katika shule inaitwa Murray Girls High School ambapo ameanza kutoka kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita na mimi vile vile nimesimama hapa nimesoma Murray Girls High School kutoka kidato cha tano mpaka kidato cha sita.

[Applause]

Kwa hivyo nafikiri vile niko mchapa kazi hata mama Roselyn ni zaidi yangu. Twende kwenye *knowledge*, nina imani kuu kwamba mama Roselyn ako na *knowledge* ya kutosha ama uzoefu wa hio kazi ambayo anatakikana apewe kutokana na stakabadhi zake vile zinavyojuza hizo zenyewe, hizo stakabadhi tunaona amehitimu, amesoma ana kila kitu ya kupasa yeye kupata kazi hii. Nikimalizia *integrity*, tunaona katika mambo ya makortini kushtakiwa nini mama Roselyn yuko msafi hana shida zozote na korti. Kwa hivyo mimi nimesimama kuunga mkono mama Roselyn aweze kupata nyadhifa hii, aweze kusaidia wananchi wetu wa Mombasa ahsanteni sana mubarikiwe sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Okay, the seconder of the Motion Honourable Pamela?

**Hon. Ojala:** Thank you Mr. Speaker for this opportunity. Before I proceed to give my contribution, I would like to welcome the students from The Smart Academy, feel at home and feel free. Mr. Speaker, I do not want to argue more because I just stand to support this nominee Roselyn Randu, because when you look at the history and the education background, it speaks for itself. Mr. Speaker, I just stand to support thank you.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Leila Nyache?

**Hon. Nyache:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kunipa fursa hii. Kwanza natanguliza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Pili, nachukua fursa hii kukaribisha watoto wetu wa kutoka Wadi ya Kongowea shule ya Smart Start Academy, karibuni sana watoto mujisikie muko Bungeni la Mombasa karibuni sana ila nitawaambia mudumishe nidhamu kwa walimu na wazazi na mambo yenu yataweza kufunguka karibuni. Ahsante Mheshimiwa Spika kwanza nimesimama kuunga hoja hii iliyokuja na Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu Mheshimiwa Katana nataka niwapongeze pamoja na Kamati kwa kuweza kumpiga msasa huyu dada Roselyn Randu aweze kuwa *Chief Officer* wa idara ya elimu, nawapongeza sana kwa sababu dada huyu hata mimi nimemjua kitambo. Ni msichana ambaye ni mkakamavu sana na pia ni msichana ambaye anasikiza na ana hekima, ni msichana mwenye heshima zake na pia nikiangalia kwa upande wa masomo Mheshimiwa Spika, amehitimu kabisa kupitia masomo yake kwa sababu amepata a *Master Degree of Education in International Management and Policy from Birmingham University...*

---

[Interruption]

Mheshimiwa Spika, ebu niachane ahsante Mheshimiwa Spika amehitimu pia yuko na Bachelor ya Education Arts from Kenyatta University. Kwa hivyo mimi naona amehitimu kwa sababu katika tajriba yake ya masomo anama *Degree* na *Masters* amesomea maswali ya *Education*. Kwa hivyo na yeye mwenyewe pia tunampasisha hapa awe Chief Officer wa *Education*. Kwa hivyo hii masomo yake pamoja na yeye mwenyewe imeingiana kabisa Mheshimiwa Spika na huyu dada anafaa katika hii *docket* ya *Chief Officer* ya Elimu. Ningeomba wenzangu tushikane pamoja tuweze kumpitisha Madam Roselyn Randu aweze kuwa *Chief Officer* wa Elimu, aweze kuchapa kazi kama vile tunamjua anavyochapa kazi kwa sababu, ameshawahi kuchapa kazi katika Bunge hili letu katika Kaunti Assembly ya Mombasa pia ashawahi kufanya kazi. Kwa hivyo tunaomba tumpitisha aendele na kazi yake kama vile vile anavyochapa kazi ahsanteni sana na ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Kai Sylvester?

**Hon. Kai:** Shukran na labda pia niungane na wenzangu kuwakaribisha wanafunzi wetu ambao wameweza kutoka Wadi ya Kongowea, ninajua kwamba labda kupitia Bunge hili kuna yule ambaye anaweza akatamani baadaye kuwa mwanasiasa mwadilifu, kama tulivyo katika Bunge hili. Mimi sina mengi Mheshimiwa Spika kwa sababu huwa ninaamini sana kwamba ndugu yangu Mheshimiwa Allen Katana wakati wowote anapofanya kazi yake huwa anaifanya kwa uangalifu....

[Applause]

Anaifanya kwa uadilifu na vile vile kwa tajriba hivyo kubwa. Hivyo basi niseme ya kwamba japo mimi sio mmoja kati ya wale ambao waliweza kumpiga msasa, lakini kupitia rekodi yake ya kimasomo, kupitia pia ule utajiri ambao yuko nao nikilinganisha na miaka yake, inanipa sababu ya kutosha ya kwamba huyu dada yetu atakuwa ni mgwana na kiukweli, haya ndio mambo ambayo tunayaangalia katika uongozi. Hivyo basi nisiwe mwingi wa maneno bali nikaweze kumtakia dadangu Roselyn Sidi Randu kila la heri katika majukumu yake mapya ya kuhakisha kwamba, anaweza kuisongeza mbele taaluma ya elimu katika mji wetu na Kaunti yetu tukufu ya Mombasa ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Mwaka Mwalundonda?

**Hon. Mwaka Bakari:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii nami niweze kuchangia kulingana na *nominee* huyu Bi. Randu. Mwanzo nataka kusema karibuni vijana wa shule ya Smart mujisikie nyumbani na muweze kulisoma somo la leo, muweze kulikariri vizuri mukienda kuulizwa huko shule muandike insha muandike vizuri. Nataka kusema Bi. Randu ni mama, si msichana kama Mheshimiwa Leila alivyoserma kwa sababu naona hapa ni 1966 labda mimi nimemzidi na miaka miwili dadangu. Kwa hivyo si msichana isipokuwa ni mama ambaye amebobea kulingana na tajriba zake za kielimu nazona hapa sitaki kuziregelea sana kila mtu yuko na daftari yake ambayo anaona. Pili, nataka kusema Bi. Randu ni mama ambaye ameweza kuhudumu katika County Service Board ya hapa Mombasa na vile vile kwa kazi yake ambayo ni nzuri, na ndio naona leo hii amepigwa msasa na Kamati ya Elimu.

Vile vile hata mimi, naunga mkono kulingana na tajriba za elimu zake na uzoefu wa kazi yake aliyoifanya katika wakati alipokuwa yuko katika Public Service Board. Nataka kusema mimi mwenyewe najivunia kama mama, mama mwenzangu kupata fursa hii na najua penye mama pana maendeleo. Nashukuru ahsante sana Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa wenza tuweze kupitisha *nominee* huyu wetu aweze kuwa Chief Officer wetu wa Elimu.

[Applause]

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Leader of Majority?

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika nasimama kuunga mkono hoja ya uteuzi wa afisa mkuu katika kitengo cha elimu daktari Randu. Mheshimiwa Spika, kama awali nilivyosema ni kwamba afisa wakuu ni wafanyikazi wa Bodi ya Huduma za Umma katika Gatuzi na Bodi hii inaongozwa na sheria katika uteuzi wa maafisa hawa na miongoni wa sababu ambazo Bunge linaruhusiwa kupinga uteuzi ni iwapo hakukuzingatiwa thuluthi mbili za jinsia moja, hakukuzingatiwa maswala ya makabila machache katika Gatuzi na vile vile kuangalia utamaduni wa uhalisia wa Gatuzi lenyewe. Kwa hivyo nimpongeze mstahiki Gavana na bodi yake katika kupendekeza jina, hii ni katika kuongeza idadi wa maafisa wakuu, kina mama na kuhakikisha ya kwamba sheria ya thuluthi mbili imeweza kuzingatiwa. Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu sisi kama Wabunge kuunga mkono kwa sababu hapa kwa kipengele kilivyo ni kwamba sheria imeweza kuzingatiwa lakini pia kuna mzungumzaji aliyetangulia kusema kwamba sheria inasema, asilimia 30 ya waajiriwa wawe wametoka nje ya Gatuzi lile.

Hii ni kwa sababu Jumba hili ni la sheria na kumbukumbu nimfahamisha tu Mheshimiwa ya kwamba ni sehemu 65(a) ya sheria za Ugatuzi na sheria hii inasema ya kwamba asilimia thelatini ya makabila madogo wanaoishi katika Gatuzi sio watu wanaotoka nje ya Gatuzi. Kwa hivyo hii izingatiwe ya kwamba makabila madogo yanayoishi katika lile Gatuzi ndio imesema angalau asilimia thelatini iweze kufikiwa Mheshimiwa Spika na sivyo kama ilivyonukuliwa ya kwamba hiyo wametoka nje ya Gatuzi hili. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika sisi kama Mombasa tunajivunia ya kwamba kila kabila katika jamhuri yetu ya Kenya linaishi katika sehemu hii; wako wale walio wengi, wapo walio wachache lakini wote katika Gatuzi letu na wanapatikana na katika uteuzi wa mstahihiki Gavana aliweza kuzingatia hilo. Kwa kuzingatia wanaoishi haijalishi alipozaliwa, haijalishi alipotoka lakini kwa wakati huu ni kwamba wanaoishi makabila yanayoishi katika Gatuzi letu la Mombasa, ahsante Mheshimiwa Spika naunga mkono.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. I now call upon the mover of the Motion to respond. Put into consideration the issue of Members, you need to respond the question from Honourable Kai.

**Hon. Katana:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa nafasi hii tena. Zaidi niwapongeze Waheshimiwa wenzangu hata wale ambao matumbo yao kidogo yalikuwa yamechemka, nawashukuru kwa kuwa wameunga mkono ofisa huyu. Kuhusiana na maswala fulani ambayo Waheshimiwa wenzangu wameyaweke, kama Mheshimiwa jina lililoandikwa pale katika wanakamati waliopitisha kama Mheshimiwa Patrick Mbelle Mumba, nataka niweke wazi ya kwamba Bunge hili halina Mheshimiwa anayelitwa Patrick Mbele Mumba, ni makosa tu kidogo ambayo ni ya kibinadamu ndio tuliweza kunakili jina hilo Mumba. Kwa hivyo nafikiri Mheshimiwa hapo nimemuweka sawa.

Pia Mheshimiwa Spika niruhusu nigusie kitu ambacho kikienda katika kumbukumbu za Bunge hili kabla kuwekwa sawa huenda siku za usoni kikaja kikaleta matatizo. Mheshimiwa Spika, ni hoja iliyotajwa na Mheshimiwa Madialo pamoja na Mheshimiwa Mwaura wa Kongowea ya kwamba hawaelewi panapotajwa watu wetu nataka kuliweka wazi kwamba tukisema watu wetu inamaanisha watakapo kuwa wamekubalika na kupata nafasi hizi za kazi bila shaka, hawa ni watu wetu na watakuwa wakifanyia kazi Bunge letu la Kaunti. Kwa hivyo haya maswala ya kusema itagawanya watu kwa misingi ya kikabila kama Mheshimiwa kufikia sasa hajajijua yeye ni wa Mombasa basi yeye ni wa matatizo. Kila mtu aliye Mombasa na sisi kama viongozi watu hawa Mheshimiwa Spika ni watu wetu na swala ambalo limegusiwa na Mheshimiwa ninae mheshimu sana Mheshimiwa Kimari amenidhalilisha na alikuwa ameambiwa awe ataliweka wazi hili! Lakini hakuliweka wazi kwa sababu ya kumbukumbu ya Bunge hili; Mheshimiwa Spika amesema ukweli, si kwamba sikusoma sana kama daktari Randu yeye ni alikuwa aseme kwamba mimi sijafikia kisomo cha Mheshimiwa Daktari Randu. Lakini, mbele ya wanafunzi kuambiwa hukusoma kabisa inakuwa ni matatizo na sitaki kuendelea kuzidi hapo Mheshimiwa Spika, sina lengine la kuongea kuhusu Daktari Randu lakini nataka kuwashukuru Waheshimiwa wenzangu kwa hekima ambayo Mwenyezi Mungu amewapa, na kwa jumla kwa kauli moja tumependekeza kwamba ni vizuri tumpitishie kiongozi huyu ili watu wetu wakaweze kunufaika, nakushuru Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Members. I now stand to put the question that the Motion by Honourable Allen Katana, on adoption of report on the vetting of Dr. Roselyn Randu, the nominee for the position of Chief Officer Education be approved by this Honourable House in the same terms as moved?

*[Question put and agreed to]*  
*[Applause]*

Honourable Members, the Motion by Honourable Allen Katana Chairperson Committee on Education and Digital Transformation, on adoption of report on the vetting of Dr. Roselyn Randu, the Nominee for the position of Chief Officer Education is adopted by the House. Yes, Clerk?

Yes Clerk.

### **MOTION**

ADOPTION OF REPORT ON THE VETTING OF MRS. RUKIA ABDURAHMAN - THE NOMINEE FOR THE POSITION OF CHIEF OFFICER GOVERNANCE

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, Vice Chairperson Committee on Appointments and the Majority leader.

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Mr. Speaker, I beg to move the following Motion that this House adopts the report on the vetting of Ms. Rukia Abdirahman, the nominee for the position of Chief Officer, Governance as laid on the Table on Tuesday 25<sup>th</sup> July, 2023. May I ask Honourable Morgan Masaki to second the Motion?

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Morgan Matsaki.

---

**The Leader of Minority** (Hon. Matsaki): I stand to second the Motion.

*[Applause]*

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Members. I now propose a question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on adoption of report on the vetting of Ms. Rukia Abdirahman the nominee for the position of Chief Officer Governance, be considered by this Honourable House in same terms as moved.

*[Question put and agreed to]*

Yes, Honourable Athman Mwamwiri please proceed?

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Chair. From the proposed questions it seems that already the Motion has been passed so its worth if we proceed; it is a reservation to put a question, Mr. Speaker, the said nominee Rukia is a well-known person. Personally, I worked with her when she was the manager at the constituency office; I was also the manager at the women representative office in 2013 Mr. Speaker. So, we are birds of the same feather and seeing her in this position to me is an encouragement that at least I have a colleague who from the experience, from the position she held today she will be serving as Chief Officer in Governance. Being in this other end Mr. Speaker I assure the Members that the Committee under the leadership of the Chair Honourable Speaker we did our best and all the possible questions were asked and she proved to us that she understands her mandate and also being in the affirmative action group to us is an encouragement that the composition of this cabinet and the Chief Officers His Excellency the Governor also considered that indeed there are youths and women in those positions.

Mr. Speaker, this is an encouragement because some of us are parents and we have daughters and seeing a girl child being empowered, being encouraged and with adoption and power of this Assembly it also entails us to be proactive in raising the girl child knowing very well that they are recognized in the community, their position is reserved and they are supported in any position where need be. Also Mr. Speaker to another encouragement, this young lady at her age is almost Ksh.40 million worth so also it shows us that hard work, honesty and dedication can take you to some heights. To us those who are after us they can as well be assured that if they do their hard work honestly, they can as well make it in life not necessarily through dirty means but also through the noble way of making money. So, I ask the Honourable Members to approve this nominee so that we can proceed with services or serving our people in this great County of Mombasa. Thank you, Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Amriya.

**Hon. Amriya Juma:** Thank you Mr. Speaker for according me this opportunity to also make my meaningful contribution towards the nomination of Ms. Rukia for the position of Chief Officer. Mr. Speaker, I am also a Member of this Committee, Appointments Committee and I was present during the interviews for the nomination and clearly as the Majority Leader has stated that Ms. Rukia is well qualified. She has an outstanding performance Bachelor's Degree of Arts and employment record also has very rich Curriculum Vitae (CV) especially she has a degree from the Kenyatta University and also pursuing her Master's degree in Strategic Management from Kenyatta University as well and also on her employment record.

The Majority Leader has stated that she is well conversant in matters of public service because she was once a state officer of the constituency office that was in Mvita constituency office. So, I am so much convinced that she is upto the task and she will ensure that the Governor's manifesto is delivered in time because we know time is of essence and she sits in the most fragile docket that is the Governor's office. They say to who much is given more is expected, so there is a lot of expectations from ourselves and the public on this said office; so, we are wishing her all the best and am supporting this said Motion. Thank you, Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Frankline Makanga.

**Hon. Makanga:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mimi nasimama kwa utangulizi kuunga mkono kuteuliwa kwa dada yetu Rukia kuweza kuwa Afisa Mkuu katika ofisi ya Gavana. Na sababu za kumuunga mkono ni kwamba tumeweza kuangalia viwango vyake vya masomo, utenda kazi wake, historia yake na yale yote yanayohusiana na ofisi hiyo. Mimi naridhika kwamba anafaa, anastahili, anatosha na kwa hivyo apewe nafasi aweze kuwahudumia wananchi wa Mombasa na pia aweze kuwa kielelezo kwa wasichana wetu katika jimbo hili kwamba inawezekana kuweza kufika viwango ambavyo amefika katika kuwafanyia wananchi kazi. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nasimama kuunga mkono.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Honourable Mohammed Hamid.

**Hon. Mohammed Hamid:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa fursa hii. Mimi ningependa kuomba Nyumba hii ama Waheshimiwa wenza tuweze kupitisha dada huyu Rukia, yaonekana wazi katika ripoti yake hii iliyotengezwa na Kamati ya kuwa ana uzoefu na ofisi hizi za serikali kwa mda mrefu. Kwa hivyo ningeliomba sote tupitische jina hili, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Hamisi Nyota.

**Hon. Hamisi Nyota:** Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. I stand to support the approval of Ms. Rukia Abdirahman in the said position. Having gone through the report am confident that the Committee having the Members they had vetted this nominee and am confident they are people who can do the thorough work. According to this report am confident that when she is given this chance having much knowledge and experience, she is able to handle this docket very well. Mr. Speaker, I have seen that she has vast experience in matter of management as she was a manager for almost close to ten years at Mvita constituency. It is high time we give this lady an opportunity to work in the office of the Governor so that Governors' manifesto can become a reality. This lady having much knowledge and experience I think she is the right candidate and I urge Members in this House to come together and approve this nominee so that she can start her work as soon as possible so that this County can move forward to greater heights. Thank you, Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mwalimu Makarani): Thank you. Yes, Honourable Leila Nyache.

**Hon. Nyache:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika mara nyengine tena kunipa nafasi nimesimama kuunga mkono hoja hii iliyokuja na Kiongozi wa Wengi nataka nipongeze Kamati ikiongozwa na Mheshimiwa Spika ambae ni Spika wetu na mahali alipo Spika tunajua mambo ni mazuri na yeye pia ni mtu mchapakazi, kwa hivyo hawezi chagua mtu ambae hawezi kuchapa kazi, ninawapongeza sana Kamati. Jambo lengine Mheshimiwa Spika nataka nipongeze huyu dada kupitia bidii zake za kikazi; ni mtu nimemjua kitambo Rukia Abdulrahman, nimemfahamu kitambo msichana wetu tumefanya nae kazi ya kampeni sana, alikuwa ni mkakamavu sana sana na hata alikuwa *upto date* ukisahau kitu anakukumbusha.

Kwa hivyo ni mtu ambae ana heshima zake na ana hekima na anajua watu, anajali watu, hivyo basi tunapongeza kwa hii *docket* ningomba tu Waheshimiwa wenza tuweze kupitisha kwa sababu hii rikodi yake ripoti yake muko nayo na munaona ako karibu kupata *Masters* yake na pia ako tayari na *Bachelor's Degree* yake kutoka Kenyatta University. Kwa hivyo pia kwa upande wa kazi ana ujuzi wa miaka kumi ana uzoefu wa miaka kumi katika kazi, mashirika mbalimbali na hata kazi za serikali. Napongeza na naomba jamani Waheshimiwa wenza tuweze kupitisha msichana wetu aendelee kuchapa kazi na tuweze kusaidia wana Mombasa aweze kupata hii Afisa Mkuu wa kitengo cha *Governance* na tunamtakia kila la heri. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani):** Thank you. Yes, Honourable Jactone Madialo.

**Hon. Madialo:** Mr. Speaker Sir, I stand to give my support towards this Motion. Majority Leader has told us that her net worth should be a motivation for us to work hard so for that reason because I also want to after five years be recorded to be of Ksh.50 million net worth from my 100 thousand so that is a motivation for me to support. I support.

**The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani):** Thank you, Yes Honourable Mwaura.

**Hon. Mwaura:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Hata na mimi naungana na wenzangu mkono japo nilifikiria kama nitakuwa upande mwengine lakini nimebadilika kwa sababu ya maneno ya Mheshimiwa Kiongozi wa walio Wengi kwamba tukiona mtu ana hela nyingi tufanye bidii. Na mimi pia nafanya bidii niwe na hela nyingi lakini pia japo naunga mkono niseme kuangazia kule mbele maswala mengine tutaangalia sana kwa sababu nikiangalia huyu dada amesema pesa mahali zimetoka ni kutoka kwa *sacco dividends*, kutoka kwa mazao ya kilimo na kutoka kwa *women groups* za kina mama.

Mheshimiwa Spika, niko na shida kidogo na pesa zinazotoka kwa *women group* maana najua huko ni kutoa wanatoa lakini sio kupata wanapata. Kwa hivyo ikiwa yeye ni kupata anapata pesa kutoka kwa *women group* hii inaashiria taswira tofauti sana na yale ambayo tunaweza kutazamia kutoka kwa *nominee* huyu ama kutoka kwa yoyote anayepata pesa kutoka kwa *women groups*. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nataka kusema kuendelea mbele maswala ya fedha ni ya muhimu sana ikilinganishwa na miaka ambayo mmoja ameweza kuhudumu ama kufanya kazi. Ila nasimama kuunga mkono ili na mimi kama Mheshimiwa Madialo nikitoka hii Bunge baada ya miaka minne niwe za zangu nimeweza kutafuta. Ahsante.

**The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani):** Thank you. Yes, Honourable Milka Moraa.

**Hon. Ngare:** Thank you Mr. Speaker.

I have stood to support the report that was done by the Committee that is led by our able Speaker and presented by our Majority Leader for the position of nominee, Chief Officer Governance Ms. Rukia Abdulrahman. Having looked at her academic even before the academic I have interacted with Ms. Rukia on official occasions and I have observed that she is a very determined and hard-working young girl and her records speak for itself and I think she is headed for bigger things. She already has acquired a Bachelor's Degree and now pursuing a Masters Degree in Strategic Management from the Kenyatta University. I think that is qualification enough to allow her to take this docket, also looking at the number of female Chief Officers that we have passed in this Assembly, I think we must also look at the 2/3 gender rule and for sure ensure we are in uniformity with that Article of the Constitution. So, as a fellow woman I also support that we pass Ms. Rukia Abdulrahman as the nominee for Chief Officer Governance to continue her work at the Governor's office and with that I ask our fellow Honourable Members that Ms. Rukia is qualified for this position and we should support her. Thank you so much Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes...?! No, I call upon the mover of the Motion to respond.

**The Leader of Majority** (Hon. Mwamwiri): Ahsante Mheshimiwa Spika, niwashukuru Waheshimiwa wenza kwa kuweza kuchangia. Mheshimiwa Spika, katika hoja hii kuna mambo kadhaa nimejifunza mojawapo ni ile nadharia ya kwamba wanawake ni adui wa wa wanawake wenzao. Nadharia hii naona sio ya ukweli kwa sababu wanawake wameweza kuchangia chanya kwa mwanamke mwenzao na kuweza kuuunga mkono na hii tumeiona katika uteuzi wa Mawaziri uteuzi wa ma ofisa wakuu wakiwa na mawazo chanya kwa wanawake wenzao, niwapongeze kwa hilo Mheshimiwa kuweza kuithibitishia dunia ya kwamba nadharia hiyo sio sahihi. Pili, katika kuwashukuru na pia kuwakumbusha Waheshimiwa wenza ya kwamba haijathubuthu katika dunia hii mtu kutajirika kutumia mshahara wake Mheshimiwa Spika kwa hivyo katika kuwapa ama sisi kua na ghera ya kuweza kufanikiwa kimaisha na kuwa na maisha bora ya kifedha. Vilevile pia Mheshimiwa Spika lazima tujifunze maswala ya kilimo kuwekeza, tujifunze maswala ya biashara lakini zaidi lazima tujifunze maswala ya kuwekeza maswala ya kuwekeza tujifunze maswala ya biashara. Lakini zaidi Mheshimiwa Spika tujibidiishe katika maswala ya kilimo na tusitegemee mshahara; wapo watu ambao hawajabahatika kuajiriwa katika dunia hii lakini tukiwazungumzia ni miongozi mwa matajiri wakubwa wanaotambulika katika dunia hii tofauti na baadhi yetu ambao tumekuwa katika mrengo huu wa kuajiriwa na kutegemea mshahara. Kwa hayo Mheshimiwa Spika amesema kwamba dada huyo ana shahada kutoka Kenya University kwa ajili ya kumbukumbu inukuliwe vyema kwamba ni Kenyatta, kwa hayo mengi nashukuru Waheshimiwa wenza kwa kuweza kuchangia lakini zaidi kuunga mkono uteuzi wa banati huyu katika ofisi hii kama afisa mkuu kwa serikali yetu ya Gatuzi la Mombasa. Ahsante Mheshimiwa Spika na niwatakie mchana mwema waheshimiwa wenza.

**The Deputy Speaker** (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Members, I now stand to put the question that the Motion by Honourable Athman Mwamwiri on adoption of report on the vetting of Ms. Rukia Abdulrahman, the nominee for the position of Chief Officer Governance be approved by this Honourable House in the same terms as moved.

*[Question put and agreed to]*

*[Applause]*

The Motion by Honourable Athman Mwamwiri, Vice Chairperson Committee on Appointments on adoption of report on the vetting of Ms. Rukia Abdulrahman the nominee for the position of Chief Officer Governance is adopted by the House. Yes Clerk.

### ADJOURNMENT

Honourable Members, there being no other business, the House stands adjourned until Tuesday 1<sup>st</sup> August, 2023 at 2:30p.m.

The House rose at 12:13p.m.